| NAMBA YAKO YA MTIHANI | |
|---|---|
| JINA LAKO | |
| JINA LA SHULE YAKO | |

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# KCPE 2005

## KISWAHILI

## SEHEMU YA PILI: INSHA

**Muda: Dakika 40**

**SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI**

1. Kwenye nafasi zilizoachwa hapo juu andika Namba Yako kamili ya mtihani, Jina lako na Jina la Shule yako.
2. Sasa fungua karatasi hii, soma kichwa cha insha kwa makini na uandike insha yako kwenye nafasi uliyoachiwa.

**Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu juu ya kichwa kifuatacho:**

**Malizia insha yako kwa . . . Nilishangaa nisiweze kuamini kuwa nilikuwa nimeepuka hatari hiyo. Moyoni nilimshukuru Mungu kwa kuniokoa.**

**Kijitabu hiki kina kurasa 4 zilizopigwa chapa.**

© The Kenya National Examinations Council, 2005

# KCPE 2005 KISWAHILI

## SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

**Maswali 1 mpaka 15.**

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Malkia alivua __1__ wake kichwani akamtazama kitwana huyo kwa hasira asijue la kufanya. Hakuweza kuamini __2__. "Si huyu aliyekuwa mtumishi wangu mwaminifu?" __3__ kimoyomoyo. "Kwa nini akanifanyia hivyo licha ya __4__ niliyomtendea?" Alikumbuka alivyomwokota kijana huyo akichumia chungu mekoni hana hali wala mali, akifanya vibarua __5__, __6__ mpaka akaonekana nadhifu; akampa kazi, tegemeo na usalama. "Leo hii anathubutu __7__ kiasi hiki? Ama kweli ivushayo ni mbovu."

1. A. ukanda B. utaji C. utepe D. ukosi
2. A. aliyoyasikia B. aliyasikia C. aliyeyasikia D. aliosikia
3. A. Akajisema B. Akamsema C. Akamsemea D. Akajisemea
4. A. mingi B. wengi C. mengi D. nyingi
5. A. vidogovidogo B. ndogo C. kidogokidogo D. dogo
6. A. akamtuza B. akamtunza C. akamtunzia D. akamtuzia
7. A. kumdhulumu B. kudhulumu C. kuwadhulumu D. kunidhulumu

Uhifadhi wa mazingira ni jambo __8__ sharti lishughulikiwe __9__. Kwa kuwa mazingira ni uhai, hatuwezi kamwe __10__ wito wa __11__. __12__ mitaa yetu imesheheni __13__ ya taka za kila aina. Miti imekatwa kiholela kwa minajili ya kupata mbao __14__ kutengenezea mapaa ya nyumba. __15__ na hali hii tutabakia kujuta.

8. A. ambayo B. ambaye C. ambalo D. ambao
9. A. wote B. kote C. yote D. zote
10. A. kuzingatia B. kuhimiza C. kufikiria D. kupuuza
11. A. kuzilinda B. kuilinda C. kuyalinda D. kulilinda
12. A. Hata hivyo B. La sivyo C. Kwa hivyo D. Au sivyo
13. A. matuta B. mabumba C. mabiwi D. mabunda
14. A. ya B. la C. wa D. za
15. A. Tukienda B. Tukiendelea C. Tukiendeleza D. Tukiendea

*Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.*

**16.** Baba, mama, wifi, shangazi ni *majina ya jamii.* Shungi la nywele, halaiki ya watu ni majina ya
- A. makundi
- B. pekee
- C. wingi
- D. dhahania

**17.** Chagua neno ambalo halipaswi kuwapo katika kundi hili.
- A. Kasuku
- B. Njiwa
- C. Korongo
- D. Siafu

**18.** Kukanusha kwa sentensi:
Maria ameingia darasani akanipata.
ni:
- A. Maria hakuingia darasani wala hakunipata
- B. Maria hajaingia darasani wala hajanipata
- C. Maria haingii darasani wala hanipati
- D. Maria ameingia darasani wala hakunipata

**19.** Chagua usemi wa taarifa ufaao wa: "Ukija mapema nitaweza kukutembeza humu mwetu," Fatu akamwambia.
- A. Fatu alimwambia kuwa angekuja mapema angeweza kumtembeza humu mwao.
- B. Fatu alimwambia kuwa akija mapema ataweza kumtembeza humu mwao.
- C. Fatu alimwambia kuwa angekuja mapema angeweza kumtembeza humo mwao.
- D. Fatu alimwambia kuwa akija mapema ataweza kumtembeza humo mwao.

**20.** Bainisha matumizi ya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi:
Mwanafunzi <u>huyu</u> ni wangu, <u>yule</u> pale ni wako
- A. kivumishi, kiwakilishi
- B. kielezi, kiwakilishi
- C. kivumishi, kielezi
- D. kiwakilishi, kivumishi

**21.** Tofauti ya maana kati ya <u>wanne</u> na <u>wa nne</u> ni:
- A. Wanne ni idadi ya jumla na wa nne ni idadi kamili katika orodha.
- B. Wanne ni kuonyesha sifa na wa nne ni kuonyesha idadi.
- C. Wanne ni kuonyesha idadi kamili na wa nne ni anayechukua nafasi ya nne katika orodha.
- D. Wanne ni idadi kamili na wa nne ni idadi katika orodha.

**22.** Chagua sentensi inayoonyesha <u>kwa</u> ya matumizi
- A. Ameenda kwa haraka
- B. Amealikwa harusini kwa Hamisi
- C. Tulikula wali kwa mchuzi
- D. Alienda Ulaya kwa ndege

**23.** Mahali gerezani anapowekwa mshukiwa akingojea kesi kumalizika huitwa
- A. kizimba
- B. rumande
- C. jela
- D. mahakama

**24.** Jibu la kitendawili 'Hushindana wakifuatana' ni
- A. kivuli
- B. mawingu
- C. miguu
- D. magurudumu

**25.** Chagua uakifishi ufaao wa:
Musa alishangaa lo leo umepatikana
- A. Musa alishangaa "lo leo umepatikana!"
- B. Musa alishangaa lo! leo umepatikana!
- C. Musa alishangaa, "Lo! Leo umepatikana!"
- D. Musa alishangaa, Lo leo umepatikana!

**26.** Njuga ni kwa mguu. Zulia ni kwa
- A. sakafu
- B. dari
- C. kiambaza
- D. dirisha

**27.** Panga vifungu vifuatavyo kuunda sentensi yenye maana kamili
*(i) Yanayohusu maisha yao*
*(ii) Vijana wa hirimu*
*(iii) Huwa na mazungumzo*
*(iv) Kuhusu mambo*
- A. (iv) (iii) (i) (ii)
- B. (ii) (iii) (iv) (i)
- C. (ii) (iv) (iii) (i)
- D. (i) (ii) (iii) (iv)

**28.** Chagua sentensi yenye <u>ki</u> ya kuonyesha udogo
- A. Kikoba kile kimejaa pesa
- B. Kiambaza kile kitapakwa rangi
- C. Akija kule atampata
- D. Mtoto yule amevaa Kiafrika

**29.** Wingi wa sentensi: Seremala aliitengeneza meza nzuri akamuuzia mteja ni:
- A. Seremala walizitengeneza meza nzuri wakamuuzia mteja
- B. Seremala walizitengeneza meza nzuri wakawauzia wateja
- C. Maseremala walizitengeneza meza nzuri wakaziuzia wateja
- D. Maseremala walizitengeneza meza nzuri wakawauzia wateja

**30.** Utosi ni kwa kichwa.
Kisigino ni kwa
- A. mtulinga
- B. mkono
- C. wayo
- D. goti

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31–40.*

Faraja alikuwa kainamia mashine yake ya kompyuta akifanya kazi kwa furaha. Ilikuwa siku yake ya pili katika ofisi hii kubwa. Kwa kweli, hakuna aliyeweza kufikiria kuwa kijana huyu angepata kazi nzuri kama hii. Wazazi wake, Bwana Chakavu na Bi. Tabu hawakuweza kupata elimu ya kisasa ambayo iliwawezesha marika zao kupata kazi za ajira ofisini. Wazazi hao wakabakia kufanya kazi katika mashamba na majumba ya matajiri.

Ingawa Bwana na Bi. Chakavu walijitahidi kufanya kazi, pato walilopata halikuweza kutosheleza mahitaji ya watoto wao. Licha ya kushindwa kuwapa watoto hao lishe bora, wazazi hawa waliona vigumu sana kuwanunulia mavazi mazuri na hata kuwalipia karo ya shule. Maisha kwa Faraja na ndugu zake yakawa ya taabu na mashaka.

Ni kweli kuwa Faraja na ndugu zake walikuwa maskini wa mali. Hata hivyo, vijana hawa walikuwa matajiri wa akili. Akili zao zilikuwa kama visu vikali vinavyokata kwa ncha zote. Kila mara Faraja aliliongoza darasa lake. Ndugu zake pia walipata alama nzuri. Jambo hili liliwatia wazazi wao moyo, wakafanya kila juhudi kuwalipia karo. Hata hivyo Faraja na ndugu zake walikuwa wakifukuzwa kuleta karo. Wanafunzi waliosoma na Faraja walipogundua kipawa chake, walianza kumheshimu na kumpenda. Hata wale waliomdharau kwa uhitaji wake walinong'onezana kisirisiri wasije wakamuudhi. Kwa hakika, licha ya Faraja kuwa hodari masomoni, alikuwa karimu na mnyenyekevu. Hakusita kuwasaidia wale ambao walikuwa visu butu katika masomo mbalimbali. Jambo hili lilimfanya aendelee kupendwa na wanafunzi na hata walimu.

Wahenga walisema kuwa chanda chema huvikwa pete. Juhudi za Faraja shuleni zilimpa pato; akawa mwanafunzi bora katika mtihani wa darasa la nane na kujiunga na shule moja ya kitaifa nchini. Haukupita muda kabla ya shida ya ukosefu wa karo kujidhihirisha. Bwana Chakavu akatafuta usaidizi asiupate. Faraja akaanza kuona kwamba kamba yake ya matumaini inatishia kukatika.

Hata hivyo, waliosema kuwa wema hauozi hawakukosea. Katika shule ya Faraja kulikuwa na mwanafunzi mmoja aliyewahi kusaidiwa na Faraja masomoni wakiwa shule ya msingi. Mwanafunzi huyu kwa jina Tegemeo, alikuwa na wazazi waliojiweza. Aliwaomba wazazi wake wamsaidie Faraja, nao, kwa kujua umuhimu wa kuwaelimisha vijana, walijitolea mara moja kumlipia Faraja karo hadi kidato cha nne. Haya yalimpa Faraja nguvu mpya, akazama zaidi masomoni ili kuonyesha shukrani kwa wafadhili. Aidha, aliazimia kuwatua wazazi wake mzigo wa kuwakimu ndugu zake.

Hivi sasa Faraja ni mfanyikazi wa hadhi kubwa katika mojawapo ya mashirika ya serikali. Moyoni haachi kuwashukuru Bwana na Bi. Karimu kwa wema wao.

**31.** Watu hawakufikiria Faraja angepata kazi nzuri kwa kuwa
A. wazazi wake hawakupata elimu ya marika zao
B. wazazi wake walikuwa maskini
C. wazazi wake hawakupata kazi yoyote kama wengine
D. wazazi wake walikuwa na watoto wengi.

**32.** Mambo yanayoonyesha matatizo ya akina Faraja ni
A. kutopata chakula na shida ya karo
B. shida ya karo na kutopata chakula bora
C. kutopata chakula bora na ukosefu wa mavazi
D. ukosefu wa mavazi na wazazi kuwa na pato duni.

**33.** Wanafunzi walimpenda Faraja kwa sababu
A. hakuwalaumu walipomsema kisirisiri
B. aliwasaidia ndugu zake na wazazi
C. alikuwa karimu na mnyamavu
D. alikuwa karimu na mnyenyekevu

**34.** Kitendo kisichoonyesha ukweli wa methali <u>Chanda chema huvikwa pete</u> ni
A. Faraja kuwa mwanafunzi bora katika mtihani
B. Faraja kulipiwa karo na Bwana na Bi Karimu
C. Wazazi kusaidiwa na Faraja
D. Faraja kufanya bidii kazini

**35.** Wazazi wa Tegemeo walimsaidia Faraja kwa kuwa
A. walijua umuhimu wa kusaidia
B. walijua umuhimu wa urafiki
C. walijua umuhimu wa kuwaelimisha vijana
D. walijua umuhimu wa wema wa vijana.

**36.** Chagua jawabu lililo sahihi zaidi:
Faraja alijitahidi zaidi masomoni ili
A. kuwashukuru wazazi kwa kuwasaidia nduguze
B. kuwashukuru wafadhili kwa kumsaidia
C. kuwashukuru wazazi na wafadhili
D. kuwashukuru wafadhili na kuwasaidia wazazi

**37.** Kulingana na kifungu matendo yanayoonyesha kushughulikiwa kwa watoto ni
A. kutowafukuza shule na kujitahidi kuwasomesha
B. kujitahidi kuwasomesha na kuwalipia karo
C. kuwalipia karo na kuwasaidia katika masomo
D. kuwasaidia katika masomo na kuwapa lishe bora.

**38.** <u>akaanza kuona kwamba kamba yake ya matumaini inatishia kukatika</u> inamaanisha
A. amelikosa alilotumainia
B. alilotegemea huenda asilipate
C. alilotarajia halipatikani kabisa
D. aliloazimia halitakuja

**39.** Kulingana na taarifa hii, maana ya <u>visu butu</u> ni
A. wanafunzi wasiofanya vyema masomoni
B. visu visivyokata
C. wanafunzi wasiotia bidii masomoni
D. visu visivyopata makali.

**40.** Kichwa kinachofaa zaidi kwa taarifa hii ni
A. Faraja hupata shida
B. Ni muhimu kusaidia
C. Tusikate tamaa
D. Umaskini huumiza

*Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 41–50.*

Hivi majuzi palizuka patashika katika vituo viwili vya polisi. Watoto wanaojulikana kama chokora waliwaonyesha polisi kisanga. Walipanga njama za kutapakaza vinyesi katika vituo hivyo vya polisi.

Kisanga hiki kilichukuliwa na wengi kama ujinga, kichekesho na uchafu. Hata hivyo, tendo hilo likipigwa darubini linaweza kuzua mambo mengi ambayo yanapaswa kumulikwa. Hebu tujiulize kwanza: Ni nani aliye na akili timamu ambaye angeenda haja kubwa, kisha achukue kinyesi hicho na kukishika na kukitumia apendavyo bila kuhisi kinyaa? Bila shaka jibu la swali hili unalijua fika.

Kisanga kama hicho huwa na chanzo chenye kina kirefu ambacho kisipochunguzwa kwa undani kinaweza hata kuangamiza nchi. Ajabu ni kuwa jamii yetu imejaa mapuuza kuhusu maswala ya watoto. Watoto wanachukuliwa kuwa hawana uwezo wa kujiamulia, kwa hivyo hawashirikishwi katika maswala mengi yanayohusu maisha yao. Kutokana na hali hii jamii imeshindwa kutambua shida za watoto hawa. Watoto wanapoona kuwa wanapuuzwa huamua kuchukua hatua mbalimbali kuishinikiza jamii kuwashughulikia. Kisanga kilichotokea katika vituo vya polisi ni njia mojawapo tu ya kuonyesha uchungu mkubwa walionao watoto hawa. Jambo la kusikitisha ni kwamba wengi wetu hatujatafakari na kuvivumbua vilio vya watoto hawa. Badala yake, tunawachukua kama punguani, wachafu, wezi . . . . Wengi wapitapo karibu nao hufunga pua zao na kuchepukia mbali wakiwaambaa kama wagonjwa wa ukoma. Ni binadamu wachache sana ambao huthubutu kuwakaribia na kuwapa msaada. Hakuna wengi wanaosutwa na nafsi zao na kujishughulisha kusugua bongo na kujiuliza kwa nini watoto hawa wakageuka kuwa hivyo. Ukweli ni kuwa, hawa ni binadamu wenzetu. Kila binadamu anapaswa kujaliwa maslahi yake. Watoto wana haki ya kuishi hata kama ni maskini. Wanastahili kupendwa na kutimiziwa mahitaji yao ya kimsingi.

Jamii ina jukumu la kutafuta suluhisho la kudumu kuhusiana na hali ya watoto hawa. Kuna haja ya kuwa na mipango kabambe ya kukabiliana na tatizo hili sugu. Kwanza itabidi waketishwe kitako na kuhojiwa ili chanzo cha matatizo yao kijulikane. Huenda baadhi ya matatizo yao yanayowafanya wawe mitaani ni kukosana tu na wazazi, ndugu au walimu. Wengi wao wakipata washauri watakaowapa nafasi ya kujieleza, wataweza kukubali kurejea makwao. La sivyo wakiachwa waendelee kuzurura mitaani watakutana na 'walimu' wabaya wa kuwapotosha zaidi. Ikumbukwe kuwa baadhi ya watoto wanaotoroka kwao, wafikapo mijini hukumbana na matatizo makubwa zaidi ya yale yaliyowatoa nyumbani. Ingawa wengi wao wangependa kurudi kwao, hawafanyi hivyo kutokana na woga na aibu. Watoto hawa wakiwahiwa mapema watarudi nyumbani na kuishi vyema. Chuma kiwahi kingali moto.

Aidha, watoto wanaopelekwa kwenye vituo vya kurekebishia tabia hawafai kuachwa kukaa bure. Wataanza kujitafutia 'vibarua' na tutarudi palepale. Idara ya watoto na wahisani wengine washirikiane kuwapa makao ya kudumu na huduma kulingana na umri na vipawa. Tatizo la watoto hawa ni swala nyeti ambalo haliwezi kuachiwa polisi au mabaraza ya miji pekee. Ni tatizo la jamii husika. Ikumbukwe kuwa, watoto wanazo haki zao nyingi na zinafaa kutambulika zaidi ili tusije tukayaona ya Firauni.

41. Kisanga kinachozungumziwa hapa ni
   A. watoto kufungiwa kwa sababu ya kutapakaza kinyesi
   B. jamii yetu kupuuza shida za watoto
   C. kutapakaza kinyesi katika vituo viwili vya polisi
   D. jamii kuona kitendo cha watoto kama kichekesho.

42. Bila shaka jibu la swali hili unalijua fika ina maana
   A. watu wenye akili punguani hujitapakaza uchafu.
   B. mtu mwenye akili timamu hawezi kujitapakaza uchafu.
   C. kuna wapendao kushika uchafu bila kuhisi kinyaa.
   D. hakuna punguani apendaye kushika uchafu.

43. Kulingana na kifungu, mambo makuu yanayowaathiri watoto ni
   A. shida zao kutotambuliwa, kutoshauriwa, kutoshirikishwa katika maamuzi
   B. kujiamulia mambo, kupuuzwa, kunyanyaswa
   C. kuwaambaa, kuwazibia pua, kuyajali maslahi yao
   D. kutowasomesha, kutoyajali matakwa yao, kuwaona kama punguani

44. Vitendo vya watoto havipaswi kudharauliwa kwa kuwa
   A. ni njia ya kuondoa hasira zao
   B. ni kuonyesha kuwa wameonewa makaoni
   C. ni kuonyesha kuwa wanadharauliwa nyumbani
   D. ni njia ya kutaka kuelezea matatizo yao

45. Kulingana na kifungu hiki, ni sentensi ipi ambayo si sahihi?
   A. Wachache hujisuta nafsi na kutafuta chanzo cha shida za watoto
   B. Wachache huwafungia pua na kuchepuka
   C. Kuzurura mitaani kutasababisha watoto kupotoshana
   D. Watoto wakiwa pamoja wanaweza kufanya makubwa.

46. Kwa mujibu wa taarifa hii, suluhisho la tatizo la watoto wa mitaani ni
   A. kusaidiwa ili waweze kujirekebisha
   B. kupewa kila wakitakacho
   C. kupewa makao na kusomeshwa
   D. kusaidiwa kila wanapotaka msaada.

47. Maana ya tusije tukayaona ya Firauni ni
   A. mambo mengi zaidi yanaweza kuonekana
   B. mambo yaliyotarajiwa yanaweza kutokea
   C. mambo ya kusisimua yanaweza kuonekana
   D. mambo makubwa zaidi yanaweza kutokea

48. Neno kina kama lilivyotumiwa katika kifungu ni
   A. chenye shida
   B. chenye uzito
   C. cha kutisha
   D. cha muda

49. Patashika maana yake ni
   A. kupata na kushika
   B. kuaibishana
   C. kuvurugana
   D. kupakazwa uchafu

50. Anwani inayofaa zaidi kuelezea kifungu hiki ni
   A. Shida katika vituo vya polisi
   B. Utatuzi wa visanga nchini
   C. Usipoziba ufa utajenga ukuta
   D. Akumulikaye mchana usiku hukuchoma